**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**684** **VITENDO VYA KUJIFUNZA SANAA**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2012**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja mambo manne yanayoweza kumsaidia mtoto wa Elimu ya awali kupenda kuchora.

2. (a) Eleza maana ya kuchapa.

   (b) Bainisha hatua tatu za kuchapa sarafu ya Shilingi Mia Mbili kwa njia ya kusugua.

3. Tofautisha maumbo ya msingi na maumbo ya upili.

4. Kwa nini vitendo vya ufinyanzi vinasisitizwa vifundishwe kwa watoto wa Elimu ya awali? Toa sababu mbili.

5. Taja vyombo au ala nne zinazoweza kupiga melodia katika muziki.

6. Taja hatua nne za utengenezaji wa yai kwa kutumia udongo wa mfinyanzi.

7. Taja sifa nne za sanaa za maonesho.

8. Ukiwa ni mwalimu wa somo la Vitendo vya Sanaa mtarajiwa, taja misingi minne ya kuzingatia katika uundaji wa vifani mbalimbali.

9. Bainisha tofauti mbili kati ya soga na vichekesho.

10. Chora kielelezo cha kuimba solfa " do mi so do" na "so la ti do" katika ngazi ya kupanda na kushuka.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia mifano, fafanua manufaa sita anayopata mtoto wa Elimu ya Awali anaposhiriki katika uundaji wa vifani mbalimbali.

12. Uigizaji wa kutumia vitendo na maneno na uigizaji bubu unaathiri sana ujifunzaji wa watoto wa Elimu ya awali. Jadili.

13. Kwa kutoa hoja tano, eleza umuhimu wa kujifunza kupaka rangi kwa watoto wa Elimu ya awali.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

14. Kwa kifupi, eleza umuhimu wa unamu mwororo na kwaruzi. Toa hoja mbili kwa kila unamu.

15. (a) Eleza mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandaa andalio la somo.

(b) Kwa kutoa hoja tatu, elezea umuhimu wa andalio la somo kwa mwalimu wa watoto wa Elimu ya awali,

16. Kwa kutumia mifano ya umahiri wa Upakaji Rangi, eleza vipengele vifuatavyo vya Andalio la Somo:

(a) Umahiri mkuu

(d) Shughuli za kutendwa na mtoto

(b) Umahiri mahususi


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org